



DSPACE

<https://dspace.org/>

**Ni Kufuwata Sati za Majagina wa Isimu: Mayelezo Maae
Kuhusu Jinakabila Bajuni, Gunya wa ani ya Kenya**

Mohamed Karama

2026

<https://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/1182>

GOMBO LA ISIMU TUMI

NI KUFUWATA SAŢI ZA MAJAGINA WA ISIMU

DKT. MOHAMED KARAMA, UNIVERSITY OF KABIANGA

Mayelezo Mačace Kuhusu Jinakabila Bajuni, Gunya wa Pani ya Kenya

Mnamo Mači 2007 niliwasili Lamu Museums, Lamu kama Afisa wa Research Institute of Swahili Studies of Eastern Africa (RISSEA), wakaŵi huwo, kurugenzi la Makumbušo ya Kiŵaifa ya Kenya (NMK). Katika mkutano mmoja na maafisa wenġine wa makumbušo hayo, ka bahaŵi nzuri, Mmambasa mimi, mġeni wa sehemu hizi, likaniŵoka neno “waGunya” nikimaaniša wat^hu waišiyo sehemu za visiواني Lamu. Papo hapo nikasahihišwa na afisa menzanġu, “usiwaite wat^hu wa huko waGunya, hawapenġi. Waite waBajuni”. Nikajifunza. Sikuuliza ka nini. ManaTikTok Saloowechu09 naye katika usanifu wake ametunġa video inayooneša unenibezi la neno “Gunya” na kulitiya kina ča “kunya” ambalo piya ni madarau ya “kiteŵro ča kenra čoo kikuba”. Kenye somasoma zanġu kuhusu waSwahili nikakutana na Derek Nurse, manaisimu mŵajika wa kiSwahili, naye akalisema kabisa katika ŵanbihi ya moja ya makala yake kuwa neno “Gunya” lina hasasi ya kudarau wat^hu wa jamii ya waBajuni. Isiŵoše, nilipokuwa nafanya usaili, wala si uŵafiŵi, niliwauliza wazee wawili watatu waBajuni kuhusu jinakabila “gunya” walilikataa na kusema wawo ni waBajuni na si waGunya. Makala haya mafupi yaŵafafanuwa k^hit^hu kičace kuhusu majinakabila haya: Bajuni/Bajun na Gunya ili tupate kuyafahamu ni ka nini jinakabila moja lakubalika na lenġine lakataliwa, na lenġine lakataliwa-kukubalika na jamii hiyo hiyo ya waBajuni. Ka kuŵowa ušahiŵi wa kiHistoriya na kilisimu tuŵaoneša kuwa majinakabila yoŵe mawili—Bajuni na Gunya—ni ya wat^hu waitawo waBajuni na kamba katika kipinri fulani majinakabila haya yali(na)tumika sawiya bila ya kuwa na hasasi za madarau.

Učanġanuzi wetu uŵatumiya Uŵaraŵibu wa Ulinġaniši na Isimu Historiya, mbinu ambazo hudadisi maneno yanavofanana na menġine katika luġa moja ao mbili na kuŵowa maamuzi yanayooneša mŵagusano wa luġa hizo mbili na hivo jamii za luġa hizo. Menġi ya tuŵakayoyaeleza humu yanatokana na nadariyatete na masimulizi yaliyomo kenye maanġiko. Tuŵajaribu kuhakikiša masimulizi hayo ka kupitiya maanġiko menġine na piya kurejeleya makamusi yanayoteġemewa ili kupunġuza ao konrowa mlemeyo wowoŵe wa mtizamo wetu. Tuŵayačanġanuwa maneno “Bajuni” na “Gunya” kama yanavoelezwa kenye makamusi na namna mapisi ya Afrika Mašariki yalivovumbuwa maneno haya. Učanġanuzi wetu uŵakuwa wa kisinkroniya na wala hauŵotizama namna maneno hayo yalivobaŵilika katika mpito wa wakaŵi. Katika makala haya neno kabila liŵatumika ka maana ya jamii pana ya wat^hu wa sehemu fulani na wala si ka maana finyu ya jamii kimbari ao kiukoo. Viyambiši /wa-/ , /ki-/ , /u-/ , na /-ni/ vinapoambišwa na maneno Bajuni na Gunya, ka kiSwahili Sanifu, yaŵamaaniša jamii yenyewe, luġa yawo, mila yawo, na sehemu waŵokako mŵawaliya. Jamii hii ya waBajuni yapatikana kenye paa za Kusini ya Somalia na Kaskazini ma Kenya na visiwa vilivopakana na mambawo huu. Mayelezo yetu yaŵajikita katika waBajuni wa Kenya tu ka sababu ya eneyo lawo lipo humu na piya maanġiko tuŵakayotumiya yamekita sana katika Kenya. Taŵaraji ufafanuzi wetu waweza kutumiwa kuwakiliša waBajuni kokot^e ulimġuni.

Jinakabila Ba-Jun-i/Ba-Jun:

Kuna wataalamu waliyotanguliya ambawo wamebainiisha jina hili laṭokana na neno lipi. Nurse (2013) na Nurse & Mahazi (2024) wanasema kuwa waBajuni hujiita wa-T^{hi} k^{huu}, wa-Gunya, na huita ka jina *al Jazira* lakini hupendeleya jina Bajuni. Nurse (1994) aliyaṇḍika jina la kabila hili namna wanavoliṭamka wenyewe, Vabajuni. Burton (1922) aliyeleza kuwa Ba-gun lina maana ya “kabila la wat^{hu} weupe”. Annachiara (2020) akinukuu kuṭoka Grotanelli (1968, uk 12) anaeleza kuwa Bajuni ni jina la wat^{hu} wanawojulikana ka jina Bani Juni wa Arabuni kusini haswa Yemen. Sacleux (1891/1939) anaeleza kuwa Bajuni ni jina walilopawa ni waArabu na waSwahili wa Kusini kumaaniisha waSwahili wanaoiṣi Kisiwa ḥa Paṭe na paa jirani nako. Horton & Middleton (2000, uk. 64) wanadokeza kuwa Baḍuys/Bedouin laweza kunasibiṣwa na usuli wa jinakabila Bajuni. Allen (1993, uk.180) ana hakika kuwa Bajuni laṭokana na Baḍui ao Baḍuj lenye kunasibiṣwa na Bedawi(n) jina wanaloita wahambe walokataa uIslam huko Arabia. Hali kaḍalika, katika Kusini ya Banaaḍir, waBajuni walikuwa wakijiita Baijun (Banaaḍiri0, n.d); “waṭakuja” iṭafsiṣiriwa ka kiSwahili hafifu kuṭoka kiArabu. Katika juhudi hizo za kila mṭaalamu kupambanua usuli wa jinakabila hilo inadhiṣirika maṭegemeyo ya mayelezo yawo kamba ni jina la kunasibiṣwa na wat^{hu} kuṭoka nje ya Afrika ao/na ni ya luḡa ya kiArabu pasi na ufungamaniṣo wowoṭ^{he} na Afrika, na piya kulazimiṣa uwafiki wa nyusuli nyengine; kinyume na asemavo Nurse (2013, uk 2) kuwa waBajuni waliḥukuwa majina yawo kuṭoka ka wavyele ao mahali waṭokako. Sibina hilo, kani waBajuni hujulikana ka wa-T^{hi} k^{huu} linaloṭokana na “nḥi k^{huu}” ambayo tuṭakuja kiyeleza ni ipi katika sehemu ijayo. Kama ilivo, katika Paṇi ya Nyali (Horton & Middleton, 2000, uk. 10)—sehemu za Mambasa, Malinri, mpaka Vaṅga kuna waMviṭa, waKilinrini, waḤaṅgame—majinakabila yaliṭokana na sehemu waṭokako wenyeji hawo.

Ka mintoṛafu ya mayelezo ya Nurse kuhusu majinakabila yaṭokako, ufafanuzi wetu wa usuli wa jina hili Ba-Jun-i/Ba-Jun (pana umuhimu wa kuligawa hivi kimofimu) tuṭatumiya njiya mbili kulifafanua: kutumiya makamusi ya luḡa ya kiArabu na uHistoriya ya Maṣariki ya Afrika. Tuṭatumiya, mosi, luḡa ya kiArabu ka sababu jina lenyewe limekaribiyana na mofolojiya ya kiArabu lakini sisi tuṭaelemeya kenye uAfrika zaiḍi kuliko kuwa ni jina la kuṭoka nje ya Afrika. Kiyasi ya ufafanuzi huu ni kama neno “Swahili” laṭokana na kiArabu “sahil” lenye keleza mambawo uliopakana na waṅwa wa Sahara (Karama, 2021). Pili, ufafanuzi wa kiHistoriya uṭatupa sisi muḥṭaḍa wa kelewa matukiyo yaliyoṭokeya Afrika haṭa yakasababiṣa jina hili Bajuni kuḍihiri.

Katika makala haya tumekuwa tukiyaṇḍika Ba-Jun-i/Ba-Jun ka sababu katika mofolojiya ya kiArabu kiyambiṣi /ba-/ kikija kenye nomino pekee ya jinakabila mara nyingi mofimu hiyo huwaṣiriya “wat^{hu} wa” ao “kina”; aḡalabu wat^{hu} kuṭoka Yemen. Huku Mambasa kuna makabila wanawoita BaYusuf, BaHassan, BaAlawy. /al-/ piya hutumika ka mofimu hiyohiyo—al Kiṇḍy, al Nahḍy, al Ahḍaly. /-i/ kenye Bajuni ni kulifanya neno hilo liwe la kiSwahili ka kufuwata mpaṅgiliyo wa silabi ya kiSwahili kiṣiya na silabi wazi kama “Ṣukurani”; na Bajun limebaki la kiArabu ka kukosa /-i/ miṣoni. “Jun”, kimaoni yetu, nriyo mzizi wa jina hilo ka kiArabu na humaaniṣa: kufiḥa (Mustafa, 2004, uk. 140; Baalbaki, 1995, uk. 85; Kamali, n.d); weusi (Mustafa, 2004, uk. 149). Piya “jun” humaaniṣa “mkono wa bahari (*inlet*), ḡuba (*gulf*), ḍaka baharini (*bay*)” (Baalbaki, 1995, uk. 439). Ḡuba ni sehemu ya paṇi iliyoṇḡiya nrani kama ḍaka na kuyafinika maji ya bahari; ao ni mkono wa bahari ambawo piya huruhusu maji ya bahari kiṅḡiya nrani arḍini. Kuṭokana na fafanuzi hizo mbili: weusi ambayo nriyo raṅgi ya mili wa muAfrika; na sehemu ya ḡuba ambako nriko maskani ya waBajuni—Kisiwa ḥa Paṭe—kukawapa jina lawo “wat^{hu} wa ḡuba, mkono wa bahari”. Maumbile ya arḍi hapo yaṭadhiṣiṣa kamba kisiwa hiḥo kiko ka nrani kuliko veṅine ambavo vimeṭapakaa baharini. Tusiṣahau piya, kuliṅgana na Allen (1993, uk. 50), moja katika sehemu zinazodaiwa ilikuwako Ṣuṅḡwaya ni arḍi mkabala wa kisiwa ḥa Paṭe. Ka

hivo, jinakabila Ba-Jun-i lina maana ya “wat^hu wa ġubani”, “wat^hu weusi” ao piya “wat^hu walofiċika”, pengine na bahari kuu.

Njiya ya pili ya kufafanuwa jinakabila Ba-Juni (taliyaṇḍika kihivi si kama hapo awali) linatokana na mapisi ya uhamiyaji uliyofanyika katika enzi za zamani Afrika. WaBajuni wanajulikana kuwa wawo ni waBantu ka sababu luġa yawo ya kiSwahili ni kizaliya ċa Mame-Bantu. WaBantu asili yawo ina nadariyatete mbili kuhusu kitovu ċa walipoanziya kuhama. Kuna nadariyatete ya Greenberg inayokisiya kuwa waBantu waliġoka Afrika Maġaribi sehemu za Cameroon na Nigeria kusini kujiya huku Mašariki ya Afrika (Massamba, 2017). Massamba anafafanuwa tena nadariyatete nyengine iliyoenrelezwa ni Guthrie inayokisiya waBantu asili yawo waliġoka Kongo na kuġapakaa kujiya Mašariki ya Afrika. Nadariyatete zothe mbili zimetumiya upekuzi wa luġa za makabila yanayozuṇḡumza luġa zinazofanana na kuġowa mahiṭimišo yawo. Phiri (1982, uk. 12) wa Historiya ya Nguni anašikiliya hoja za masimulizi ya kijaḍi ya wenyeji wa kabila hili kuba lililoko Kusini ma Afrika na namna walivohama kuġoka Kaskazini Mašariki ya Afrika na kufika Afrika Kusini na makabila mengine kuġapakaa tena kenra kaskazini na kuseleleya Malawi na Tanazania ka jinakabila waNgoni. Uhamiyaji huu wa waBantu kuhamiya Cameroon na kufikiya Mto Juba, kupitiya ama Maġaribi ya Kenya ao kupitiya kaskazini ya Tanzania na kufikiya mto huwo piya yameelezwa ni Massamba (2017, uk. 128). Ka mayelezo haya, waBantu walifika na kuseleleya Kaskazini Mašariki ya Afrika halafu wakaġawanyika tena kelekeya kusini. Sehemu hii ya Kaskazini Mašariki ya Afrika kuliḡana na mayelezo yaliyoko Wikipedia ni eneo lililoko baina ya Afrika Kaskazini na Afrika Mašariki na hujumuiša nči za Pembe ya Afrika (Djibouti, Eritrea, Ethiopia, na Somalia). Mto Juba uko kusini ma Somalia na yasemekana Šuṇḡwaya (nči ya asili ya waBantu na hivo waSwahili wakiwamo waBajuni) ilikuwako kati ya mto huwo na mto Sabaki uliyoko upa wa Kenya. Ka hivo waNguni waliiši hapo ka miyaka halafu wakasoṇa ċini kujiya Afrika Kusini.

Phiri (1982) anasema hawa waNguni waliita abe-Nguni, vaNgoni na majirani zawo (uk. 61). WaBajuni taweza kusema ka kuwa wawo nriyo wanawoiši katika sehemu ya Mto Juba na Mto Sabaki, bila kuyaepuka makabila mengine ya waBantu, na jinakabila lawo kufanana na la waNguni—Ba-Jun-i/vaBajuni na abe-Nguni/vaNguni/vaNgoni—basi yamkini waBajuni nriyo waNguni. Kani tukiṭeṇḡaniša wa-ba-Jun-i na wa-Nguni na tunapoonrowa /N/ katika Nguni (kama ṇgoma na goma, ṇdude na dude) mofimu zinazosaliya ni “Juni” na “Guni” na /dz/ huweza kupišana kuwa /g/ ka mfano /msiṇdzi/ na /msiṇgi/. Hivo basi, maana ya Bajuni ni wat^hu weusi, wat^hu wanawoiši kenye sehemu iliyofiċika na bahari k^huu ikisaḍifu sawasawa na eneyo la Kaskazini Mašariki ya Afrika. Pili, Phiri anafafanuwa kamba makabila ya kiNguni yanawoneša ukuruba wa mṭagusano ka sababu ya mfanano wa luġa zawo. Yeye na Massamba (2017) wanaġowa mifano inayooneša kuwa kiSwahili (ambayo nriyo luġa ya waBajuni) inafanana sana na isiZulu luġa ya moja ya makabila ya waNguni ya Afrika Kusini hivi sasa. Mfano wa Phiri (uk 12) ni:

Zulu	Swahili
ukulala	kulala (<i>to sleep</i>)
ingoma	ngoma (<i>music</i>)
muluṇḡu	mzuṇḡu (<i>white person</i>)
imali	mali (<i>property</i>)
unina	nina (<i>mother</i>) nimeeṇgeza mimi

Katika mifano hiyo kuna mšabaha wa karibu sana baina ya kiSwahili na kiZulu. Kuġokana na mfanano huu wa kiluġa, Phiri anasema jamii hizi zilikurubiyana haġa katika makazi na lazima palikuwa na maiṇḡiliyano ya kijamii haġa ya kuwowana. Si ajabu wakaṭi jamii mbili zinapoṭagusana mpaka zikaweza kukopešana maneno yaonekana kulikuwa na mamana mzuri baina yawo. Je, makutano haya yalikuwa wapi ikiwa si huko Kaskazini Mašariki ma

Afrika ambako nriko baina ya Mto Juba na Mto Sabaki. Je, taweza kupendekeza kuwa hiyo *Tʰi kʰuu* (nči *kʰuu*/kuba/ʈukufu) nriyo nči walikokutaniya makabila mēngi yaliyoṭokeya Cameroon kupitiya Uganda, Maḡaribi ya Kenya wakapatikana Aba-Luhya, Aba-Gusii, Aba-Kuriya (Ndeda, 2019) na kufikiya Bajuni (Kaskazini Maṣariki ya Afrika)? Je, ni hakika alivosema Sacleux (1891/1939), *Tʰi Nene* (nči kuba barani) ni nči waiṣiko waGunya (uk 413)? *Ukʰuu* ao ukuba huu waṭambiya nini kuhusu wiṅgi wa makabila ya waBantu yaliyokuwa yakiiṣi hapo? Ao, labḍa, Bajuni-ni ambalo nrilo jina la nči walimokuwa wakiiṣi waBajuni ni kufu ya kiNguni ambaḇo kinaḇo mofimu /-ni/ ya mahali inayosemekana ni sifa kuu ya kiSwahili (Huffman, 2004) na kuṭokana na mofimu hii ikawa waNguni nriyo waBaJuni? Tusisahau, kuna sehemu na kisiwa chata Ngumi (Nurse & Mahazi, 2024) na piya kuna watʰu waita waNgumi Bajunini. Ukuruba huu wa Ba-Juni na abe-Nguni ni uṣahiḍi mmojawapo wa usuli wa jinakabila Bajuni.

Jinakabila Gunya:

Kama tulivokiṣasema huko nyuma, waBajuni hawapenḍi kīta jina hili. Sababu mojawapo ni kamba waBajuni walimaaniṣa “watuma” ka baadi ya watʰu waiṣiyo hapo kawo (Nurse, 2013). Walakini ṭangu zama za Krapf (1882, uk. 20), alimeleza Mgunya kuwa mtʰu aiṣiyo kenye sehemu za kisiwa ḇa Paṭṭa na Mto Juba. Hali kaḍalika, ni jina watumiyalo waSwahili wa Kusini (Uṅguja, Mambasa) kuwaita watʰu waiṣiyo kenye arḍi ya Siwe [Siyu] na Mto Juba (Steere, 1919, uk. 339) ao watʰu wa kaskazini ya Mambasa (Stigand, 1915, kur 3, 53). Ka hivo, ṭangu kale neno hili lilikuwako na lilitumika kiyusahihi kama alivofanya Sacleux (1891/1939) kenye kamusi lake la kuṭegemewa—aloikusanya Uṅguja—aliiweka lahaja kiGunya kuwa marejelezi ya maana za maneno ya kiSwahili kuliko kiyita kiBajuni.

Tukirejeleya mapisi ya Upa wa Afrika Maṣariki pamekuwako na ṭawala za waAfrika kaḍimu, waPortugezi, waArabu, waIngereza. Na kila ya ṭawala hizo kulikuwa na mifanyiko inayostahiki na isostahiki kīta uṭawala. Čembeleḇo Phiri (1982) waAfrika waliṣi ka uṭangamano na majirani zawo ṭangu azali na walipogombana hawakuwafanya wenziwawo watuma bali waliwafanya walipe koḍi ya uliṇzi. Wanapoono mahala hapo hapawaweki ṭena basi waliyamuwa kusonga mbele kuṭafuṭa pema penye amani. Utuma unajiṭokeza ka kukiṭiri wakaṭi himaya za waṭawala hawo walipopapiya uṭajiri ulokuwako Afrika. Walitumiya mabavu kuyapata mali hayo na wakiwamo watuma. Hiči ni kisa katika hiṣṭoriya ya waAfrika na hakifutiki. Tumeeleza hayo ili mukṭaḍa wa neno Gunya upate kujulikana.

Uṭawala wa waPortugezi Afrika uliyanza mnamo 1498 wakaṭi Vasco da Gama alipokita hema lake huku na kuṭaka kuṭawala biyaṣara pame na watʰu. Mmoja wa magavana wa kiPortugezi, Nuno da Cunha aliṭawala kanziya Lamu haḍi Pemba. Aliweka koḍi ya mapato na uṭawala wake, kama wenziye, ulikuwa muwovu. Sisi hatulenḡi uṭawali wake sisi talenḡa jina lake, Cunha /kunya/. Katika kiSwahili fonimu /k/ huweza kupiṣana na /g/ ka mfano neno /kiza/ kuṭamka /giza/ na maana ikawa haikubaḍilika. Ka hivo, asili mojaapo ya Gunya ni Cunha, mṭawala wa kiPortugezi alokuwako huku uSwahilini. Kuṭokana na uṭawali wake muwovu nriposana, na jina lake likapata čembe za ubaya. Fauka ya hayo, neno cunha, kuliḡana na Wiktionary, lina maana ya kabari (*wedge*) inayotenganiṣa vitu viwili.

Tukiwa hapohapo kenye kiPortugezi, neno cunha katika luḡa za huko kawo (Galacia) lina maana ya ku-guna yaani kukasirika. Ṭamko /guna/ huweza kuwa gunya katika kiSwahili kwa mofimu ya kauli ya kuteṇreṣa kama ilivo /ona/ huwa /onya/ katika kauli hiyo. Nriposana, Burton (1922) akasema maana ya gunya ni kugawanya, piya ni kabila la watʰu watesi, akiyelezeya hulka yawo. Nurse (1985) na Nurse & Mahazi (2024) nawo piya wanayezeza fasili mojaapo ya neno gunya ka neno la kiPortugezi, Nurse alilipata ka Allen, *vanagunes* /vanaguneṣ/, ketu sisi limaaniṣalo ṭabiya ya ubabe “povu” (Deepseek, 2026). Katika kulazimiṣa maana, kama tulivosema hapo mbeleni, Allen (1993, uk. 158) ameligawa

vanagunes kuwa *vana gunes* na akasema, akimnukuu mMišeni Wakefield kuwa wat^hu hawo wa upwa Afrika Mašariki waliita waBunya yaani “wezi”, neno Bajuni [kisisi gunya] laṭokana na hiyo *gunes*.

Hali kadhalika, katika usaili wangu wa wazee waBajuni nilowauliza, mmoja alinipa fasiri ya ka nini hawapendi kitwa waGunya ka sababu Gunya ni nchi si kabila. Mfano alonipa ni kama jinanchi Kenya, hakuna kabila la Kenya isipokuwa kuna makabila zaidi ya arubaini nranime na kila moja lina jinakabila lake. Ka kengezeya, Njogu (2024) amekisiya usuli wa neno gunya laṭokana na jina la kiyongozi mmoja wa Bajunini akiita Ngunya Mgunya (walodhukuru Vave kwa Nurse [1994] hawakusema Ngunya lilikuwa jina la kiyongozi wawo) ambaye alikuwa mBajuni mbihi anawahangaiša wavuvi hadi sehemu za Zanzibar; Nurse (1994, uk. 57) kwenye tanbihi amefasiri Ngunya kuwa ni “jina la kutukuza”. Fasili hii sisi taikubali ikiwa italega kenye tabiya ya uhasama ya jagina huyo, lakini tahoji kamba neno gunya laṭokana na Ngunya Mgunya ka sababu mbili: manzo jina hilo lina “M-gunya” ambapo hicho ni kiSwahili Sanifu ka kiyambihi ngeli /m/. Tena, haiyamkiniki kiyongozi wa Kaskazini MaGunyani/Bajunini liwe jina lake ni la lugha ya Kusini Zanzibar. Pili, neno Ngunya halitamki /ngu.nya/ ka sababu yeye Njogu, ao (w)alomfafanuliya, piya yamkini (w)amelikuta neno/jina hilo katika maandiko ya watagulizi, ka mfano, Nurse (1994, uk. 63) limeyandika Ngunya na humo hutamka /n.gunya/ kenye masimulizi ya “Suyu a Vabajuni” msitari wa 13 linalorejeleza “mt^hu wa Gunya”. Sasa tushike ni /ngu.nya/ au /n.gunya/ nriyo usuli wa jinakabila Gunya? Suwala hili lajibika kamba pana shida ya usawi na, *kama ninavosema kila siku, pana haja ya kiSwahili cha kiKenya kiyandike upya*. Kwa mfano, neno “Ndodhi” limeyandika hivo kengine lakini ukija ka Nurse (1994, uk. 56-7) limeyandikwa “Nḍodhi” ka namna wanavolitamka waBajuni wenyewe; ijapokuwa, ka kuḡafilika labda, ukurasa 64 Nurse ameliyandika “Ndhodhi”. Alakulihali, kuṭokana na fasili hizo za neno gunya: kukasirika, kunasibišwa na watawala wa kiPortugesesi, wezi, kiburi, kabari, wabihi na wat^hu waso na kabila, ni wazi neno gunya lilipata atari za uhasi. Sibina, waBajuni hawapendi kita waGunya.

Swali la kujiuliza ni ka nini waBajuni hawahawa wanakataa kita waGunya lakini wanakubali na wanalitumiya jina la sehemu waliyoko bila ya kuwa na kinyezi wanapolitaja ao wanaponasibišwa nako hata hivi leo? Jina la sehemu waliyoko waiyita wenyewe Magunyani /ma-Gunya-ni/, kaskazini ma pani ya Kenya. Tukiličunguza neno hilo tutaona limo katika ngeli ya JI-MA nriposana /ma-gunya/. Pili, ile /-ni/ ni kielezi cha mahali chenye kashiriya ni nomino ya mahali: ma-hospitali-ni, ma-soko-ni, ma-duka-ni. Aidan, mifano yote tuliyoṭowa kuhusu /ma-, -ni/ ni maneno yaliyokopa kuṭoka luḡa nyengine na kingizwa kiSwahilini. Mgawo huwo unatuwoneša mzizi ni upi na katika neno ma-gunya-ni mzizi ni gunya. Na kuṭokana na mayelezo yetu gunya lina asili ya kiPortugesesi lenye kashiriya tabiya ya wat^hu lakini piya jina la gavana mPortugesesi, Nuno da Cunha.

Kulingana na Deepseek (2026) Cunha ni katika majina ya wat^hu wataukufu huko uPortugesesi na walipawa nyadifa za uwongozi wakati wa ustawi wa uPortugesesi. Mayelezo ya mapisi ya waPortugesesi Afrika Mašariki na Afrika ka ujumla ni ya uwovu ulopita mipaka. Walisagasaga miji, mali na wenyeji wa upa huu bila huruma wala kinyezi (Boxer & Azevedo, 1960). Juu ya hayo, kuna maneno maḡaḡe ya kiPortugesesi yaliyopenya kenye kiSwahili: kanju, ukaju, korošo, meza, foronya, mvinyo – kuhusu ḡakula na semani za majumbani ka waSwahili hata mṭafiti huweza kujiuliza kama ilikuwa ni ubaya tu uliyowasifu waPortugesesi. Makala haya si ya mjadala huwo wa uzuri au ubaya wa waPortugesesi, lakini kuṭokana na mayelezo yaliyomo kenye Nurse (1994, uk. 66) na Allen (1993, uk. 119) tutaona waSwahili walikuwa na ṭangamano fulani zuri na waPortugesesi. Katika masimulizi aliyorekodi Nurse (1994), mBajuni aliwayeleza kuwa majumba, minara, magofu, misikiti(?) na uhifadi wa waBajuni uliṭokana na usaidizi wa waPortugesesi. Piya kulingana na Allen (1993, uk. 119), ijapo ka kupiḡa, kuna ukoo wa waFamau unawojitaja kamba asili yawo ni

waPortugesesi na hujiita Bunu Reno “ukoo wa kiReno/Portugesesi”. Pingamizi yake ni Bunu kiIsimu haiwezi kugeuka na kuwa Bani “wat^hu wa”. Lakini kiSwahili ča kikawaiđa mt^hu kīta ao kujiita “bunu” yaweza piya kumaaniša “watoto wa” ambayo itakuja karibu ya “bani” ka wingi. Kutokana na učanganuzi huu basi, taweza kukisiya kuwa waBajuni, na si wawo tu, katika miyaka miya mbili ya utawali wa waPortugesesi waliingiliyana na waPortugesesi na, pengine, wakaowana na kuzaana, sembuse wakakubali nči yawo, mpaka leo, waiyita mar-gunya-ni bila ya kuwa hasasi wala wakiŋzani.

Hiŋimišo:

Makala haya yamečanganuwa majinakabila ya Bajuni na Gunya ka mințarafu ya kiIsimu Historiya na Uțaratibu wa Ulinganiři ili keleza nyusuli za majina hayo. Lengo k^huu lilikuwa ni kujaribu kuwaweka waBajuni kēnye miđani ya uAfrika wawo wanawoutamini pame na mapisi yawo. Učanganuzi wetu ulirejeleya makamusi ya kiArabu, kiSwahili na zaiđi, maandiko yaliyopo kuwahuu wanađi hawa wa Afrika Mařariki. Muktađa wa kihistoriya piya ulitiliwa maanani na ukatufunuliya meŋgi kuhusu maneno na wat^hu wenyewe. Tumejuwa kupitiya makala haya Bajuni ni jinakabila la wat^hu weusi, waliyoțangamana na makabila meŋginayo ya waBantu na wanaenreleya kuiři katika Kaskazini ya Pani ya Kenya huku wakijitambuliša ka alama za maingiliyano na wat^hu waliyokuja kuțangamana nawo kama waArabu, waPortugesesi, na waAfrika wenziwawo.

Marejeleo:

Allen, J. V. (1993). *Swahili origins: Swahili culture & the Shungwaya phenomenon*. James Curry Ltd.

Annachiara, R. (2020). Connected Islands: Swahili intellectual history from Kenya’s Lamu archipelago. Africa Studies Centre Leiden.

Baalbaki, R. (1995). *Al Mawrid: A modern Arabic-English dictionary*. Dar El-Ilm Lilmalayin.

Banaadiri0, (n.d). Bajun ballads: Somali songs in Swahili. Tiktok.
<https://www.tiktok.com/@banaadiri0/video/7602813371108363550>

Boxer, C. R. and Azevedo, C. (1960). *Fort Jesus and the Portuguese in Mombasa*. Hollis and Carter.

Burton, J. (1922). Report on the Bajuni Islands. *The Journal of the East Africa and Uganda Natural History Society*, 17, 24-28.

DeepSeek. (2026). Conversation on Bantu language terminology, Galician-Portuguese etymology, and East African coastal geography [Large language model].
<https://www.deepseek.com>

Grotanelli, V. L. (1968). Somaliya: Antologia storico-culturale. Bagiuni.No. 5.pdf

Horton, M. & Middleton, J. (2000). *The Swahili*. Blackwell Publishers Limited.

Huffman, T. N. (2004). The archaeology of the Nguni past. *Southern African Humanities* 16, 79–111.

Karama, M. R. (2021). Kugeuza đira ya toponimi Swahili. *The University of Kabianga Newsletter*. University of Kabianga.

- Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. Trubner & Co.
- Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili: Mtazamo mpya 100KK hadi 200BK*. Kiswahili Development Limited.
- Mostafaloay89. (n.d). Sheikh Said Kamali maana Junn. Tiktok.
<https://vm.tiktok.com/ZS9JNerjSqstP-z1bjio/>
- Mustafa, I. (2004). *Mu'jam Al Wasit* (Intermediate dictionary) (4th ed). Al-Shorouk National Library.
- Ndeda, M. A. J. (2019). Population movement, settlement and the construction of society to the east of Lake Victoria in precolonial times: the western Kenyan case. *The East African Review*, 52, 83-108. <https://doi.org/10.4000/eastafrica.473>
- Njogu, K. (2024). Mohamed Kombo: The Bajuni Spoken Word Artist. Katika K. Njogu & A. L. Omar (wah.). *Bajuni: Land, Language and Orature*. Twaweza Communications Limited.
- Nurse, D. & Mahazi, J. (2024). Bajuni – A Language Peninsula. *Journal of Language Contact* 16, 216–234.
- Nurse, D. (2013). Bajuni Database. Newfoundland Memorial University.
- Nurse, D. (1994). Historical texts from the Swahili coast. *AAP*, 37, 47-85.
- Nurse, D. (1985). Denticity, areal features, and phonological change in northeastern Bantu. *Studies in African Linguistics* 16 (3), 243-279.
- Phiri, D. D. (1982). *From Nguni to Ngoni: A history of Ngoni exodus from Zululand and Swaziland to Malawi, Tanzania and Zambia*. Popular Publications.
- Sacleux, C. S. (1891/1939). *Dictionnaire Swahili - Francais*. Institut d' Ethnologie.
- Saloowecheu09. (2025, September, 23). Mgunyaaa Kunyaaa: Vurunyaaaa viazii. Tiktok.
<https://vm.tiktok.com/ZMHK7GeKkEyoa-Mh6Kx/>
- Steere, E. (1919). *A handbook of the Swahili language as spoken at Zanzibar*. Society for Promoting Christian Knowledge.
- Stigand, C. H. (1915). *A grammar of dialectic changes in the Kiswahili language*. Cambridge University Press.
- Wikipedia.org (2026). Northeastern Afrca. https://en.wikipedia.org/wiki/Northeast_Africa
- Wiktionary. (2026). Etymology cunha. <https://share.google/fwHL4MtBCF57MuGk6>

Šukurani: Asanteni nyot^he mulonisaiḍiya kjuwa k^hit^hu kuhusu maḍa hii. Haswa Wakili Siham binti Seif, na Dkt. Kathryn Coney-Ali ka viṭabu vako ulivonizawaḍiya. Allah awajazii kheri nyot^heni.

Kauli Mtakaso: Mayelezo yaliyomo humu ni yangu na si ya UoK wala Idara yetu. Kuhusu makala haya, na Elimu ka jumla, wasiliyana nami mkarama@kabianga.ac.ke.